Mwanadamu Anatakiwa Afanye Nini Ili Aokolewe

na

Ellis P. Forsman

Mwanadamu Anatakiwa Afanye Nini Ili Aokolewe

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Mwanadamu Anatakiwa Afanye Nini Ili Aokolewe

Yohana 8:32

Mara nyingi tunajifunza hatua muhimu juu ya somo hili. Leo, tutajifunza katika mtazamo wa jumla.

Hebu tuzingatie kile ambacho mwanadamu anapaswa kufanya ili aokolewe.

Mwanadamu anapaswa kutambua kitu

Ujinga hakutoi hudhuru.

Mdo. 17:30, "*Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu.*"

Kukiwa na ujinga, je ni nani aliye na kosa, Mungu au mwanadamu?

Mwanadamu ndiye mwenye makosa; hivyo basi, ili kuepuka ujinga mwanadamu lazima ajifunze.

Mwanadamu lazima atambue ukweli.

Yoh. 8:32, "*Mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru.*"

Ukweli kuhusu mtu binafsi. Rum. 3:23, "*Kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*"

Ukweli kuhusu Mungu. Rum. 11:22, "*Tazama basi wema na ukali wa Mungu; kwa wale walioanguka, ukali, bali kwako wewe wema wa Mungu, ukikaa katika wema huo; kama sivyo, wewe nawe utakatiliwa mbali.*"

Tumaini kuhusu Kristo.

- Mt. 1:21, "*Naye atazaa Mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.*"
- Ebr. 5:8-9, "*Ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mates ohayo yaliyompata; naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii;*"

Tumaini katika injili. Rum. 1:16, "*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*"

Mwanadamu lazima aamini kitu

Hatuwezi kuamini kila kitu tunachokisikia.

Ambacho mtu anaamini ni cha muhimu.

- 2 Thes. 2:11, "*Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo.*"
- Ebr. 12:1-2, "*Basi na sisi pia kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.*"

Makosa haijawahi kutokea kuwa mazuri kama ukweli.

Mfano: Hawa aliamini makosa.

Mdo. 16:31, "*Wakamwambia mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako yote.*"

Tuna mianya tuliopewa katika vifungu vingine vya maandiko.

Mwanadamu lazima ahisi kitu

Huzuni ya Mungu. 2 Kor. 7:10, "*Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti.*"

Wale waliokuwepo siku ya Pentekoste walihisi kitu. Mdo. 2:37-40, "*Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi.*"

Baadhi ya ganzi iliyopita (wamepoteza hisia yao). Efe. 4:19, "*Ambao wakiisha kufa ganzi wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya uchafu kwa kutamani.*"

Sauli wa Tariso alihisi kitu. Mdo. 9:1-6, "*Lakini Sauli, akizidi kutisha na kuwa kuwauwa wanafunzi wa Bwana, akamwendea kuhani mkuu, akataka ampe barua ya kwenda Dameski zilizoandikwa kwa masinagogi, ili akiona watu wa Njia hii, waume kwa wake, awafunge na kuwaleta Yerusalemu. Hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski; ghafula ikamwangaza kote kote nuru kutoka mbinguni. Akaanguka chini akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, mbona waniudhi? Akasema u nani wewe Bwana? Naye akasema Mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe. Lakini simama uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda.*"

Wengi wanaanguka au hawajaokolewa kwa sababu hawana hisia.

Mwanadamu lazima akiri kitu

Sio hisia zake – kama ndivyo, tutakiri aibu.

Hujaokolewa bado, maana kukiri kunamwongoza mtu katika wokovu.

Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"

Lazima umkiri Kristo.

- Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"
- Mt. 10:32, "*Basi kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni.*"

Kukiri ni nini?

- Mdo. 8:37, "*Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana. Akajibu, akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu.*"
- Mt. 16:15-19, "*Akawaambia nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simoni Petro akajibu akasema, wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akamwambia, Heri wewe Simoni Baryona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda. Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni;*

na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni."

Mwanadamu lazima afanye kitu

Wokovu ni kwa neema.

- Efe. 2:8, "*Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutoka na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu.*"
- Gal. 5:6, "*Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa , bali imani itendayo kazi kwa upendo.*"

Sauli aliokolewa kwa neema, lakini bado aliambiwa kufanya kitu.

Mdo. 22:16, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*"

Maandiko yanatufundisha kusikia, kuamini, kutubu, kukiri, na kubatizwa.

Mwanadamu lazima avumile kitu

Kuna aina mbili za wokovu.

- Kwa wageni
- Kwa Wakristo waliotenda dhambi.

Tunapaswa kuvumilia:

Taabu. 2 Tim. 2:3, "*Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu.*"

Mabaya. 2 Tim. 4:5, "*Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiza huduma yako.*"

Majaribu. Yakobo 1:12, "*Heri mtu astahimiliye majaribu; kwa sababu akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaandalia wampendao.*"

Baadhi wanavumilia kwa kitambo, alafu baadaye uhamishwa.

Marko 4:14-19, "*Mpanzi huyo hulipanda neno. Hawa ndio walio kando ya njia lipandwapo neno; nao wakiisha kusikia, mara huja shetani akaliondoa lile neno lililopandwa mioyoni mwao. Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye miamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neno, mara hulipokea kwa furaha; ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu*

muda mchache; kisha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara hujikwaa. Na hawa ndio wale wapandwao penye miiba; ni watu walisikiao lile neno, na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tama za mambo mengine zikiingia hulisonga lile neno, likawa halizai."

Hitimisho

Je umetimiza mahitaji ya Bwana?

Anakuhitaji ufanye kitu; alafu damu ya Kristo itakusamehe,

Jinsi gani mtu anafanyika Mkristo? Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane.

- **Imani.** Ebr. 11:6, "*lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa katika elimu ya juu (nilikuwa kati ya miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na wa kwangu, akaniambia kuwa haamini kwamba kuna Mungu. Kwa vile nilikuwa nimesha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kuwa anaweza kuona kuwa kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kama anaamini kuwa kuna Mungu. Lakini ili awe sehemu sahihi, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri Mungu atamruhusu kwenda mbinguni (kama kuna mbingu), na sio motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haiendi hivyo. Unapaswa umwamini kwa moyo wako wote bila hivyo huwezi kumpendeza."

- **Kutubu.** Mdo 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Mdo. 11:18, "*... Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima</u>.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na ukafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani ya nyumba hii!" hivyo unachukua simu yako ya mkononi, taratibu unawapigia polisi, ukiwaambia kuwa kunamwizi ndani ya nyumba yako, na unawapa anuani ya nyumba yako. Kidogo unawasikia wamefika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "Samahani; Samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na sio kwamba ameiba. Katika toba ya kweli, mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena na anataka kubadili

maisha yake ili kwamba asije akaiba tena. Hiyo ndiyo toba ya kweli. Ni badiliko la akili inayoleteleza badiliko la tendo. Hicho ndio tunatakiwa kufanya kabla hatujafanyika Wakristo.

- **Kukiri.** Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Angalia kifungu hicho hapo juu kwamba imani (kuamini), roba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamaanisha kuelekea kitu fulani; sio kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu hupatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa kutimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*" (Mt. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo zuri kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia alisema "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote.*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake, sio kwa sababu ni haki yetu.

  Hakika, kama hatuja batizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawaambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38). Petro, umesema sababu ya ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

  Yesu aliagiza kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Mk. 16:15-16).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*" (Mdo. 22:16).

  Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo uanaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Rum. 6:4). Utu wetu wa kale unatufia. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena;*" (Rum. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tunapobatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili kaburini kuzika na kuuwekea udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?